BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# KITABU CHA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2015

# KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# KITABU CHA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2015

# KISWAHILI

Kimechapishwa na

Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2015

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI ........................................................................................................ iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA ................................. 1

2.1 Sehemu A. Sarufi ........................................................................... 2

2.2 Sehemu B: Lugha ya Kifasihi ....................................................... 24

2.3 Sehemu C: Ufahamu .................................................................... 36

2.4 Sehemu D: Ushairi ....................................................................... 49

2.5 Sehemu E: Utungaji ...................................................................... 55

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI ........................................................................................ 57

4.0 HITIMISHO ......................................................................................... 58

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ............................................................ 59

KIAMBATISHO CHA PEKEE ................................................................. 61

# DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Kiswahili imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wathibiti ubora wa elimu, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali ya mtihani huo. Majibu ya wanafunzi katika mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo wanafunzi waliweza kujifunza kwa ufasaha na yale ambayo hawakuweza kujifunza kwa ufasaha katika kipindi cha miaka saba ya elimu ya msingi.

Katika taarifa hii, mambo mbalimbali ambayo yamechangia watahiniwa kujibu/kushindwa kujibu maswali hayo kwa usahihi yameainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa yafuatayo yamechangia watahiniwa kutokuweza kujibu maswali kwa usahihi: kushindwa kutambua matakwa ya swali, kuwa na uelewa mdogo wa mada mbalimbali katika somo; kutofahamu kanuni za lugha na matumizi ya misamiati; kutojibu kabisa baadhi ya maswali au kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo katika mtihani. Uchambuzi kwa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati watahiniwa walipokuwa wanajibu maswali yao zimeainishwa kwa kuonesha idadi ya watahiniwa waliojibu maswali kwa usahihi na walioshindwa kuchagua jibu sahihi. Aidha, idadi ya walioacha kujibu swali na ambao waliandika machaguo zaidi ya moja katika swali husika imeoneshwa kwenye jedwali au grafu katika kipengele cha majibu mengine.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kupatia ufumbuzi dosari zilizoainishwa katika taarifa hii. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa endapo maoni yaliyotolewa yatafanyiwa kazi ipasavyo, ujuzi na maarifa watakayopata wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi vitaongezeka na hatimaye kiwango cha ufaulu katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kitaongezeka pia.

Mwisho Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani, Wataalam wa TEHAMA na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii. Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu kwa ujumla ambayo yatasaidia katika kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa siku zijazo.

Dkt. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kuhusu namna ambavyo watahiniwa walijibu maswali katika mtihani wa somo la Kiswahili. Mtihani wa Kiswahili ulikuwa na maswali **50** ya kuchagua jibu sahihi ambayo yalikuwa yamegawanywa katika sehemu tano ambazo ni: Sehemu A: Sarufi; B: Lugha ya Kifasihi; C: Ufahamu: D: Ushairi na E: Utungaji. Jumla ya watahiniwa **775,276** walisajiliwa kufanya mtihani wa **PSLE 2015** ambapo miongoni mwao waliofanya mtihani wa somo la Kiswahili walikuwa **763,500** na kati yao watahiniwa **589,425** sawa na asilimia **77.2** walifaulu mtihani huo.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA

Sehemu hii inaainisha maswali yaliyoulizwa na majibu ya kuchagua waliyopewa watahiniwa. Idadi na asilimia ya watahiniwa waliochagua kila chaguo (jibu) na waliochagua jibu zaidi ya moja au kuandika mambo mengine imeoneshwa. Aidha, uchambuzi wa sababu zinazoweza kuwa zilichangia wasichague jibu sahihi zimeainishwa. Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika kila swali imewasilishwa kwa kutumia jedwali au grafu. Rangi mbalimbali zimetumika kuonesha hali halisi ya asilimia ya ufaulu, ambapo ufaulu kati ya asilimia 0 – 40 umewasilishwa kwa rangi nyekundu ikimaanisha ufaulu hafifu; 41 – 60 rangi ya njano ambao ni ufaulu wa wastani na 61 – 100 rangi ya kijani inayowakilisha ufaulu mzuri.

## 2.1 Sehemu A. Sarufi

**Swali la 1**: "Ramadhani anacheza mpira uwanjani." Sentensi hii ikiwa katika hali ya mazoea itakuwa ipi kati ya hizi zifuatazo?

A Ramadhani hucheza mpira uwanjani

B Ramadhani atacheza mpira uwanjani


C Ramadhani alicheza mpira uwanjani

D Ramadhani amecheza mpira uwanjani

E Ramadhani anacheza mpira uwanjani.

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa katika kubaini hali ya mazoea katika vitenzi. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa usahihi na watahiniwa wengi kama inavyoonekana katika kielelezo 2.1 ambapo watahiniwa 564,478 sawa na asilimia 73.93 walichagua jibu A "Ramadhani hucheza mpira uwanjani". Watahiniwa 196,965 sawa na asilimia 25.8 walichagua vipotoshi kati ya B "Ramadhani atacheza mpira uwanjani", C "Ramadhani alicheza mpira uwanjani", D "Ramadhani amecheza mpira uwanjani" na E "Ramadhani anacheza mpira uwanjani" ambavyo sio majibu sahihi kwani vitenzi katika sentensi hizo vina maumbo yanayoonesha njeo ya wakati kama vile -ta- ujao, -li- uliopita, -me- timilifu na -na- uliopo badala ya hali ya mazoea ambayo hudhihirishwa kwa kuwepo umbo -hu- katika kitenzi.

**Kielelezo 2.1**: Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo




Kielelezo 2.1 kinaonesha idadi kubwa ya watahiniwa (73.93%) walikuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu hali za vitenzi.

**Swali la 2**: "Bura yangu sibadili na rehani." Kitenzi "sibadili" kipo katika hali ipi?

A Mazoea

B Timilifu

C Ukanushi

D Kuendelea

E Shurutia.

**Jedwali 2.1**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C*** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 106,361 | 130,757 | 400,508 | 76,825 | 45,453 | 3,613 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.93 | 17.13 | 52.46 | 10.06 | 5.95 | 0.47 |

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa katika kutambua hali mbalimbali za vitenzi. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani (rejea jedwali 2.1). Watahiniwa 400,508 sawa na asilimia 52.46 walichagua jibu C “Ukanushi” ambalo ndilo jibu sahihi kutokana na kiambishi awali -si- cha nafsi ya kwanza umoja kuwa katika hali kanushi. Watahiniwa 237,118 sawa na asilimia 31.06 walichagua kati ya vipotoshi A “Mazoea” na B “Timilifu” ambavyo vyote sio majibu sahihi. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa hali ya mazoea inawakilishwa na umbo -hu- na hali timilifu inawakilishwa na umbo -me- ambayo yote hayapo katika kitenzi “sibadili”. Aidha, asilimia 10.06 ambayo ni watahiniwa 76,825 walichagua kipotoshi D “Kuendelea” ambacho sio jibu sahihi kwa sababu walishindwa kutambua kuwa kitenzi “sibadili” kinaonesha kutokuendelea kwa tendo. Watahiniwa 45,453 sawa na asilimia 5.95 walichagua kipotoshi E “Shurutia”. Watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa kitenzi “sibadili” hakikuwa na umbo linaloonesha hali ya shuruti kama vile -ki-, -nge-, ngali- na -ngeli- .

**Swali la 3**: “Babu alikuwa analima shambani.” Neno “alikuwa” ni aina ipi ya kitenzi?

A Kitenzi kikuu

B Kitenzi kitegemezi

C Kitenzi jina

D Kitenzi kishirikishi

E Kitenzi kisaidizi.

**Jedwali 2.2**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 118,933 | 89,357 | 48,758 | 133,389 | 367,697 | 5,383 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 15.58 | 11.7 | 6.39 | 17.47 | 48.16 | 0.71 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutambua aina za vitenzi. Jedwali 2.2 linaonesha kuwa idadi ya watahiniwa 367,697 sawa na asilimia 48.16 walichagua chaguo E "Kitenzi kisaidizi" ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa hao waliweza kutambua kuwa kazi ya kitenzi kisaidizi ni kutoa taarifa za ziada kuhusu kitenzi kikuu. Neno "alikuwa" linatoa taarifa kuhusu wakati wa ufanyikaji wa tendo. Kuwepo kwa kiambishi -li- katika neno "alikuwa*"* kunaarifu kuwa tendo lilishafanyika. Aidha, "alikuwa" ni kitenzi kisaidizi kwa kuwa kutokuwepo kwake katika sentensi hakuathiri maana. Uteuzi wa vipotoshi kati ya A "Kitenzi kikuu", B "Kitenzi kitegemezi", C "Kitenzi jina" na D "Kitenzi kishirikishi" uliofanywa na watahiniwa 390,437 sawa na asilimia 51.13 unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu aina za vitenzi. Kitenzi kikuu huonesha tendo linalofanyika, neno "alikuwa" haliarifu tendo hivyo linakosa sifa ya kuwa kitenzi kikuu. Pia katika aina za vitenzi hakuna "Kitenzi kitegemezi". Aidha, "Kitenzi jina" ni kitenzi kinachotaarifu kuhusu tendo. Kitenzi hicho lazima kianze na mofimu -ku- kwa mfano, kuimba au kucheza. Hali kadhalika kitenzi kishirikishi ni neno linaonesha kuwepo au kutokuwepo kwa hali fulani bila kutaja tendo halisi na neno "alikuwa" haliwezi kuwa kitenzi kishirikishi katika tungo hii kwa sababu linaambatana na kitenzi kikuu "analima".

**Swali la 4:** Katika sentensi zifuatazo ipi ina maana sahihi?

A Sikuwa najua Halima ni dada yako

B Sikujua kuwa Halima ni dada yako

C Sikuwa ninajua Halima ni dada yako

D Sikuwa ninajua kuwa Halima ni dada yako

E Sikuwa ninajua kwamba Halima ni dada yako.

**Jedwali 2.3**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 31,674 | 567,747 | 30,647 | 58,194 | 71,961 | 3,294 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 4.15 | 74.36 | 4.01 | 7.62 | 9.42 | 0.43 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika matumizi fasaha ya lugha. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa usahihi na watahiniwa wengi (567,747) sawa na asilimia 74.36 ambao walichagua jibu B “Sikujua kuwa Halima ni dada yako” kama inavyoonekana katika jedwali 2.3. Watahiniwa hawa waliweza kubaini kuwa katika lugha ya maandishi baadhi ya vipashio vinavyotumika katika lugha ya mazungumzo huweza kudondoshwa ili kupata sentensi yenye maana sahihi. Watahiniwa 192,476 sawa na asilimia 25.2 walichagua kati ya vipotoshi A “Sikuwa najua Halima ni dada yako”, C “Sikuwa ninajua Halima ni dada yako”, D “Sikuwa ninajua kuwa Halima ni dada yako” na E “Sikuwa ninajua kwamba Halima ni dada yako” ambayo sio majibu sahihi. Watahiniwa walivutiwa na lugha ya mazungumzo isiyo sanifu ambapo katika mpangilio wa maneno katika sintaksia ya Kiswahili hayawezi kufuatana kwani “sikujua” ni kinyume cha “ninajua”. Vilevile, maneno “sikuwa ninajua/najua” hudondosha baadhi ya silabi /wa/, /ni/ na /na/ kisha kuunda neno “sikujua” linalokubalika kisarufi.

**Swali la 5**: Ni neno lipi kati ya yafuatayo ni kisawe cha neno “hifadhi?”

A Weka

B Panga

C Tunza

D Ficha

E Funga.

**Jedwali 2.4**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 94,572 | 25,196 | 576,289 | 46,373 | 18,004 | 3,083 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 12.39 | 3.3 | 75.48 | 6.07 | 2.36 | 0.41 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu maneno mawili au zaidi yanayokaribiana sana kimaana. Jedwali 2.4 linaonesha kuwa watahiniwa 576,289 sawa na asilimia 75.48 walijibu swali hili kwa usahihi kwa kuchagua jibu C “Tunza”. Watahiniwa hao wameonesha kuwa wanafahamu maana ya neno “kisawe” jambo lililowawezesha kubaini kuwa kisawe cha neno “hifadhi” lenye maana ya kuweka kitu mahali pa usalama linalandana na neno “Tunza” ambalo maana yake ni kuweka kitu chini ya uangalizi ili kisiharibike. Aidha, watahiniwa 184,145 sawa na asilimia 24.12 walichagua kati ya vipotoshi A “Weka”, B “Panga”, D “Ficha” na E “Funga” ambavyo sio visawe vya neno “Hifadhi” isipokuwa ni vitenzi vinavyobainisha namna mbalimbali zinazoweza kutumika kuwekwa vitu bila kuzingatia dhana ya usalama. Kwa ujumla, watahiniwa wengi walionesha kuwa wanafahamu kisawe cha neno “hifadhi” kama ilivyooneshwa katika Jedwali 2.4

**Swali la 6**: Lahaula! Loo! La hasha! Masalale! ni maneno ya aina gani?

A Vitenzi

B Vihisishi

C Viwakilishi

D Vivumishi

E Viunganishi.

**Jedwali 2.5**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 45,732 | 520,450 | 69,940 | 71,095 | 52,366 | 3,934 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 5.99 | 68.16 | 9.16 | 9.31 | 6.86 | 0.52 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno. Watahiniwa 520,450 sawa na asilimia 68.16 walichagua jibu B "Vihisishi" ambalo ni jibu sahihi kama ilivyooneshwa katika jedwali 2.5. Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa aina ya maneno "lahaula!, loo!, la hasha na masalale! ni vihisishi kwa sababu yanafuatiwa na alama ya mshangao ambayo ni sifa muhimu ya vihisishi. Asilimia 31.32 ambayo ni watahiniwa 239,133 walichagua kati ya vipotoshi A "Vitenzi", C "Viwakilishi", D "Vivumishi" na E "Viunganishi" ambavyo sio majibu sahihi kwa kutokuwa na uelewa kuwa alama ya mshangao (!) aghalabu hubainisha vihisishi katika sentensi. Aidha, kwa kuchagua vipotoshi hivyo, watahiniwa hao wanaonesha kuwa hawana ujuzi wa kutambua aina za maneno katika lugha ya Kiswahili.

**Swali la 7**: "Ingawa walipata matatizo mengi safarini_______walifika salama." Neno lipi linakamilisha sentensi hiyo kwa usahihi?

A vilevile

B kwa hiyo

C halikadhalika

D hivyo

E hatimaye.

**Jedwali 2.6**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D** | **E*** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 58,913 | 46,837 | 52,665 | 72,171 | 529,040 | 3,891 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 7.72 | 6.13 | 6.9 | 9.45 | 69.29 | 0.51 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati na usanifu wa lugha. Jedwali 2.6 linaonesha kuwa ufaulu ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 529,040 sawa na asilimia 69.29 ndio waliojibu kwa usahihi swali hili kwa kuchagua jibu E "hatimaye". Watahiniwa hao walitambua kuwa neno "hatimaye" ambalo maana yake ni mwishowe ndilo linaloleta upatanisho wa kisarufi kwani linaendana na muundo wa sentensi husika. Watahiniwa 111,578 sawa na asilimia 14.62 walichagua kati ya vipotoshi A "vilevile" na C "halikadhalika" ambavyo sio majibu sahihi kwa kuwa maneno hayo hukaa mwanzoni mwa sentensi na kuelezea hali zingine zinazohusiana na taarifa kuu inayobebwa na sentensi. Aidha, uchaguzi wa vipotoshi kati ya B "kwa hiyo" na D "hivyo" uliofanywa na watahiniwa 119,008 sawa na asilimia 15.58 ulitokana na watahiniwa kuvutiwa na maneno hayo kwa kuwa mara nyingi hutumika

kuhitimisha tungo. Hata hivyo, maneno hayo hayakuwa majibu sahihi kwa kuwa maneno “kwa hiyo” na “hivyo” hutumika kujua namna jambo lilivyofanyika ili kuelewa zaidi na sio kuhitimisha kama yalivyokuwa matakwa ya sentensi katika swali hili.

**Swali la 8**: “Mjukuu wangu hupenda kuniamkia kila mara.” Sentensi hiyo ipo katika kauli gani?

A Kutendwa

B Kutenda

C Kutendeka

D Kutendana

E Kutendewa.

**Jedwali 2.7:** Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 91,890 | 262,811 | 63,015 | 42,349 | 299,599 | 3,853 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 12.04 | 34.42 | 8.25 | 5.55 | 39.24 | 0.51 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa wa kubainisha kauli za vitenzi. Watahiniwa 262,811 sawa na asilimia 34.42 walichagua jibu B “Kutenda” ambalo ni jibu sahihi kama ilivyooneshwa katika jedwali 2.7. Watahiniwa hao waliweza kupata jibu la swali hili kwa usahihi kutokana na uwezo wao wa kuhusisha tabia ya kitenzi cha Kiswahili ambacho kikiwa katika hali yakinifu hukamilishwa na kiambishi tamati maana -a- kama ilivyo kitenzi “kuniamki-a”. Watahiniwa 299,599 sawa na asilimia 39.24 walichagua kipotoshi E “Kutendewa” kwa kuvutiwa na kiambishi awali -ni- katika kitenzi “kuniamkia” ambacho kinahusisha mtendewa na sio mtenda. Aidha, asilimia 25.84 ambayo

ni sawa na watahiniwa 197,254 walichagua kati ya vipotoshi A "Kutendwa", C "Kutendeka" na D "Kutendana" ambayo sio majibu sahihi kwani kitenzi katika sentensi ya swali husika hakina muundo wa hali zinazoendana na vipotoshi walivyochagua watahiniwa hao.

**Swali la 9**: "Wawili wameshindwa kupanda mlima Kilimanjaro." Kiwakilishi katika sentensi hiyo ni kipi?

A Mlima
B Kupanda
C Wameshindwa
D Kilimanjaro
E Wawili.

**Jedwali 2.8:** Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D** | **E*** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 67,573 | 72,522 | 134,217 | 48,427 | 436,628 | 4,150 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 8.85 | 9.5 | 17.58 | 6.34 | 57.19 | 0.54 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua aina za maneno kwa kuzingatia mpangilio wake katika sentensi. Jedwali 2.8 linaonesha kuwa watahiniwa 436,628 sawa na asilimia 57.19 walichagua chaguo E "Wawili" ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa neno "wawili" linawakilisha nomino kapa ambayo inarejelewa mwanzoni mwa sentensi. Watahiniwa 134,217 sawa na asilimia 17.58 walichagua kipotoshi C "Wameshindwa" kwa kuvutiwa na kiambishi -wa- katika kitenzi "wameshindwa" ambacho hurejelea kiwakilishi na asilimia 9.5 ambayo ni sawa na watahiniwa 72,522 walichagua kipotoshi B "Kupanda" ambacho ni kitenzi kikuu na siyo kiwakilishi. Aidha, watahiniwa 116,000 sawa na asilimia 15.19

walichagua kati ya vipotoshi A “Mlima” na D “Kilimanjaro” kwa kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu aina za maneno kwani vipotoshi hivyo ni nomino kulingana na mpangilio wa maneno katika sentensi ya swali husika.

**Swali la 10**: “Vita ilipoanza nchini Kenya watu wote ____________.”

Kitenzi kipi kinakamilisha sentensi hiyo?

A walitweta

B walitaharuki

C walitunukiwa

D walinusurika

E walitahamaki.

**Jedwali 2.9:** Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 83,622 | 227,797 | 50,497 | 262,924 | 13,4087 | 4,590 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 10.95 | 29.84 | 6.61 | 34.44 | 17.56 | 0.61 |

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa katika matumizi sahihi ya msamiati. Jedwali 2.9 linaonesha kuwa asilimia 29.84 sawa na watahiniwa 227,797 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi B “walitaharuki” linalomaanisha kuwa na wasiwasi au mbabaiko na kutaka kujua kitakachotokea baadaye. Watahiniwa 262,924 sawa na asilimia 34.44 walichagua kipotoshi D “walinusurika” ambapo watahiniwa walivutiwa na maana ambayo ni kuepuka madhara makubwa kwa bahati. Katika hali halisi kitenzi “walinusurika” sio kikamilishi sahihi cha sentensi hiyo kwa sababu hali ya kunusurika hudhihirika baada ya jambo kufikia mwisho na sio mwanzoni kama ilivyo katika sentensi hii kwamba vita ilipoanza. Watahiniwa 217,709

**s**awa na asilimia 28.51 walichagua kati ya vipotoshi A “walitweta” na E “walitahamaki” ambavyo sio majibu sahihi kwani vitenzi hivi havikidhi vigezo vya maana ya kimsamiati katika muktadha wa sentensi husika. Aidha, asilimia 6.61 ambayo ni watahiniwa 50,497 walichagua kipotoshi C “walitunukiwa” ambacho sio jibu sahihi kwani kitenzi “walitunukiwa” maana yake ni kutoa tuzo kwa kukamilishwa vyema kwa jambo fulani. Katika hali halisi vita inapoanza watu hawawezi kupewa tuzo/pongezi bali huweza kutolewa kwa askari baada ya nchi kushinda vita.

**Swali la 11:** “Tulicheza ngoma na kuimba usiku kucha.” Katika sentensi hii watenda ni nafsi ipi?

A Ya tatu wingi

B Ya pili wingi

C Ya pili umoja

D Ya tatu umoja

E Ya kwanza wingi.

**Jedwali 2.10:** Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D** | **E*** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 146,828 | 178,059 | 80,920 | 57,941 | 294,619 | 5,150 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 19.23 | 23.32 | 10.6 | 7.59 | 38.59 | 0.68 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua maumbo ya vitenzi yanayowakilisha nafsi katika sentensi. Watahiniwa 294,619 sawa na asilimia 38.59 walichagua jibu E “Ya kwanza wingi” ambalo ndilo jibu sahihi kama ilivyooneshwa katika jedwali 2.10. Watahiniwa hao waliweza kubaini kazi ya umbo -tu- katika kitenzi “Tulicheza” kinachowakilisha mtenda nafsi ya kwanza wingi yaani “sisi”. Uchaguzi

wa kati ya vipotoshi A “Ya tatu wingi” na B “Ya pili wingi” uliofanywa na watahiniwa 324,887 sawa na asilimia 42.55 unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa kuhusu maumbo yanayowakilisha nafsi za watenda katika vitenzi. Umbo linalowakilisha nafsi ya pili wingi ni -m- na -wa- linawakilisha nafsi ya tatu wingi maumbo ambayo hayakutumika katika kitenzi cha swali husika. Aidha, watahiniwa 138,861 sawa na asilimia 18.19 walichagua kati ya vipotoshi C “Ya pili umoja” na D “Ya tatu umoja” ambavyo sio majibu sahihi kwa sababu maumbo ya nafsi za umoja -u- na -a- hayapo kwenye kitenzi cha swali husika. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni mdogo kwani asilimia 60.74 sawa na watahiniwa 463,748 walichagua majibu yasiyo sahihi jambo linaloonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa na ujuzi wa kutosha katika kutambua maumbo yanayowakilisha nafsi katika vitenzi.


**Swali la 12**: "Utundu wake ulimfanya ajulikane shuleni." Neno "Utundu" limetumika kama aina gani ya neno?

A. Kivumishi
B. Nomino
C. Kiwakilishi
D. Kitenzi
E. Kielezi.

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika matumizi ya aina za maneno. Watahiniwa 155,295 sawa na asilimia 20.34 ndio walioweza kujibu swali hili vizuri kwa kuchagua chaguo B “nomino” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa hawa wameonesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za nomino kwa kubaini kuwa neno “Utundu” ni

nomino dhahania. Aidha, watahiniwa 284,507 sawa na asilimia 37.26 walichagua kipotoshi A “Kivumishi” kwa kuwa neno utundu huweza kutumika kama kivumishi cha sifa ya nomino. Katika sintaksia ya lugha ya Kiswahili neno huwa la aina husika kutokana na nafasi ya neno hilo katika sentensi. Hivyo katika sentensi "Utundu wake ulimfanya ajulikane shuleni" nafasi ya neno “utundu” unalifanya kuwa na hadhi ya nomino kwani ni neno la kwanza katika sentensi na limefuatiwa na kivumishi kimilikishi “wake”. Aidha, uteuzi wa vipotoshi C “Kiwakilishi,” D “Kitenzi” na E “Kielezi” uliofanywa na watahiniwa 319,236 sawa na asilimia 41.81 unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu aina za maneno kama kielelezo 2.2 kinavyoonesha.

**Kielelezo 2.2**: Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo




Kielelezo 2.2 kinaonesha kuwa watahiniwa wachache (asilimia 20.34) ndio walioweza kuchagua jibu sahihi.

**Swali la 13:** "Mwanamuziki hodari aliimba nyimbo vizuri." Kielezi katika sentensi hii ni kipi?

A Hodari

B Aliimba

C Mwanamuziki

D Nyimbo

E Vizuri.

**Jedwali 2.11**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 145,263 | 118,041 | 113,271 | 55,500 | 326,744 | 4,698 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 19.03 | 15.46 | 14.84 | 7.27 | 42.79 | 0.61 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno. Idadi ya ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni wa wastani kama ilivyooneshwa katika jedwali 2.11. Asilimia 42.79 sawa na watahiniwa 326,744 walichagua jibu E "Kielezi" ambalo ndilo jibu sahihi. Kipotoshi A "Hodari" kilichaguliwa na watahiniwa 145,263 sawa na asilimia 19.03 ambacho sio jibu sahihi kwa sababu kinatoa taarifa kuhusu nomino "mwanamuziki" na hivyo neno hilo ni kivumishi. Watahiniwa 118,041 sawa na asilimia 15.46 walichagua kipotoshi B. "Aliimba" ambacho ni kitenzi. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa kuhusu tofauti ya kielezi na kitenzi hivyo kushindwa kutambua kuwa kielezi ni neno linalofafanua zaidi taarifa kuhusu kitenzi. Aidha, kipotoshi C "Mwanamuziki" ambacho sio jibu sahihi kilichaguliwa na watahiniwa 113,271 sawa na asilimia 14.84. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa neno "Mwanamuziki" ni nomino, hata hivyo kwa kanuni ya lugha ya Kiswahili kielezi hakiwezi kuwa mwanzoni mwa sentensi hiyo aliyopewa. Hali kadhalika, kuwepo kwa watahiniwa

55,500 sawa na asilimia 7.27 waliochagua kipotoshi D “Nyimbo” ambacho sio jibu sahihi kunaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kujua kuwa neno “Nyimbo” pamoja na kufuata baada ya kitenzi sio kielezi bali ni nomino kwa sababu halitoi taarifa ya namna alivyoimba bali limeeleza kipi kilichoimbwa.

**Swali la 14:** “Mgeni aliondoka alikofikia _________kuaga.” Kifungu kipi cha maneno kinachokamilisha sentensi hiyo kwa usahihi?

A licha ya

B pasi ya

C bila kwa

D bila ya

E bila na

**Jedwali 2.12**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D*** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 119,066 | 68,128 | 49,830 | 482,824 | 39,491 | 4,178 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 15.59 | 8.92 | 6.53 | 63.24 | 5.17 | 0.55 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika sarufi ya lugha. Jedwali 2.12 linaonesha kuwa watahiniwa 482,824 sawa na asilimia 63.24 walichagua jibu D “bila ya” ambalo ni jibu sahihi kwa sababu kifungu cha maneno “bila ya” hurejelea hali ya kutokutekelezwa kwa jambo fulani. Vilevile matumizi ya kifungu hicho cha maneno katika sentensi husika kina upatanisho wa kisarufi na maneno mengine yanayounda sentensi hiyo. Uchaguzi wa kipotoshi A “licha ya” ulifanywa na watahiniwa 119,066 sawa na asilimia 15.59 ambalo sio jibu sahihi kwa kuwa kifungu hicho cha maneno kipo katika hali ya

uyakinishi na upatanisho wa kisarufi utaifanya sentensi hiyo kuwa katika hali kanushi kama kipotoshi “licha ya” kitatumika. Aidha, watahiniwa 157,449 sawa na asilimia 20.62 walichagua kati ya vipotoshi B “pasi ya”, C “bila kwa” na E “bila na” ambayo sio majibu sahihi. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu muundo wa sentensi katika kuangalia upatanisho wa kisarufi.

**Swali la 15:** Neno moja linalojumuisha herufi “a, e, i, o na u” ni lipi?

A Silabi
B Konsonanti
C Mwambatano
D Kiambishi
E Irabu.

**Jedwali 2.13**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D** | **E*** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 168,650 | 46,558 | 25,581 | 18,050 | 500,005 | 4,673 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 22.09 | 6.1 | 3.35 | 2.36 | 65.49 | 0.61 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika sarufi ya lugha. Takwimu katika jedwali 2.13 zinaonesha kuwa asilimia 65.49 ambayo ni watahiniwa 500,005 walichagua jibu E “irabu” ambalo ni jibu sahihi kama ilivyo katika jedwali 2.13. Watahiniwa 168,650 sawa na asilimia 22.09 walichagua kipotoshi A “Silabi” ambacho sio jibu sahihi kwa sababu zipo silabi zaidi ya irabu ambazo zinaundwa na konsonanti na irabu na hutamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti kwa mfano, “pa”, “u” “kwa” katika neno “paukwa”. Aidha, asilimia 6.1 ambayo ni watahiniwa 46,558 walichagua kipotoshi B “konsonanti” ambalo sio

jibu sahihi kwani katika sarufi ya Kiswahili konsonanti huhusisha herufi kumi na tisa ambazo ni “b, c, d, f, g, h, j, k, l, m, n, p, r, s, t, v, w, y na z.” Uteuzi wa vipotoshi C “Mwambatano” na D “Kiambishi” ambavyo sio majibu sahihi uliofanywa na watahiniwa 42,631 sawa na asilimia 5.71 ulionesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa kuhusu matamshi (fonolojia) ya lugha kwani vipotoshi walivyovichagua havina uhusiano na herufi zilizoorodheshwa katika swali husika.

**Swali la 16:** “Kaka anapenda kujisomea chumbani mwake.” Katika sentensi hiyo kitenzi kisaidizi ni kipi?

A Anapenda
B Chumbani
C Kujisomea
D Kaka
E Kwake.

**Jedwali 2.14**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 357,039 | 70,895 | 214,487 | 45,165 | 71,404 | 4527 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 46.76 | 9.29 | 28.09 | 5.92 | 9.35 | 0.59 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutambua aina za vitenzi. Jedwali 2.14 linaonesha kuwa asilimia ya idadi ya watahiniwa waliochagua jibu sahihi ilikuwa ya wastani ambapo watahiniwa 357,039 sawa na asilimia 46.76 walichagua jibu A “Anapenda” ambalo ni jibu sahihi kwa sababu kitenzi “anapenda” kina kiambishi cha nafsi -a- na njeo ya wakati -na-. Uchaguzi wa kipotoshi C “Kujisomea” ambacho sio jibu sahihi ulifanywa na watahiniwa 214,487 sawa na asilimia 28.09. Watahiniwa hao walivutiwa na kipotoshi hicho kwa

sababu kinatokana na kitenzi “soma” lakini katika sentensi husika kitenzi “kujisomea” kina hadhi ya kitenzi kikuu. Kuwepo kwa watahiniwa 45,165 ambao ni sawa na asilimia 5.92 waliochagua kipotoshi D “Kaka” ambacho sio jibu sahihi kunaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa kuhusu aina za maneno kwa kuwa neno “kaka” ni nomino na siyo kitenzi. Aidha, watahiniwa 142,299 sawa na asilimia 18.64 walichagua kati ya vipotoshi B “Chumbani” na E “Kwake” ambavyo sio majibu sahihi kwa kuwa vipotoshi hivyo ni vielezi kwani vinatoa taarifa kuhusu kitenzi.

**Swali la 17:** “Mchezo mkali ni ule tuliocheza _______ ya Timu ya Majengo.” Neno lipi linakamilisha tungo hiyo kwa usahihi?

A zidi

B zaidi

C kabla

D thidi

E dhidi.

**Jedwali 2.15:** Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D** | **E*** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 79,518 | 78,419 | 167,820 | 31,715 | 402,959 | 3,086 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 10.41 | 10.27 | 21.98 | 4.15 | 52.78 | 0.41 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika matumizi ya sarufi ya lugha. Jedwali 2.15 linaonesha kuwa swali hili lilijibiwa kwa usahihi na watahiniwa 402,959 sawa na asilimia 52.78 kwa kuchagua jibu E “dhidi” ambalo ni jibu sahihi kwa sababu linakamilisha maana inayowasilishwa katika sentensi. Kipotoshi C “kabla” kilichochagualiwa

na watahiniwa 167,820 sawa na asilimia 21.98 sio jibu sahihi kwani kinasababisha utata katika sentensi kwa kuwa hakipambanui timu iliyocheza. Watahiniwa 79,518 walichagua kipotoshi A “zidi” ambacho siyo jibu sahihi kutokana na matatizo ya lafudhi ambapo katika lugha ya mazungumzo neno “dhidi” laweza kutamkwa “zidi” kimakosa. Uchaguzi wa kipotoshi B “zaidi” ambacho sio jibu sahihi ulifanywa na watahiniwa 78,419 ambao ni asilimia 10.27. Watahiniwa hao walivutiwa na maana ya neno “zaidi” bila ya kuzingatia upatanisho wa kisarufi usioathiri taarifa katika sentensi husika. Aidha, watahiniwa 31,715 sawa na asilimia 4.15 walichagua kipotoshi D “thidi” ambacho sio jibu sahihi kutokana na ama athari ya lugha ya kwanza (lugha mama) au matatizo katika ala za sauti zinazohusika na utamkwaji wa sauti -dhi- katika neno “dhidi”.

**Swali la 18:** Mama Ntilie akiondoka, uondoke naye. Sentensi hii ipo katika wakati gani?

A Ujao

B Timilifu

C Shurutia

D Uliopo

E Mazoea.

**Jedwali 2.16:** Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 403,884 | 76,421 | 62,914 | 166,569 | 50,943 | 2786 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 52.9 | 10.01 | 8.24 | 21.82 | 6.67 | 0.37 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua njeo za nyakati. Jedwali 2.16 linaonesha kuwa watahiniwa 403,884 sawa na asilimia 52.9 walichagua jibu A “Ujao” ambalo ndilo jibu sahihi . Asilimia 21.82 ambayo inawakillisha watahiniwa 166,569 walichagua kipotoshi D “Uliopo” ambacho sio jibu sahihi. Watahiniwa hao walionesha kutokuwa na uwezo wa kutambua tofauti zilizopo kati ya umbo la -ki- ya shuruti linaloonesha jambo litakalotokea wakati ujao na umbo la -na- la wakati uliopo. Watahiniwa 76,421 sawa na asilimia 10.01 walichagua kipotoshi B “Timilifu” ambacho sio jibu sahihi kwa sababu hakuna njeo timilifu bali hali timilifu ambayo katika sarufi ya Kiswahili huonesha jambo lililofanyika muda mfupi uliopita. Watahiniwa 62,914 ambao ni sawa na asilimia 8.24 walichagua kipotoshi C “Shurutia” ambacho sio jibu sahihi kwa sababu shurutia sio wakati bali ni hali ya tungo kuwa na shuruti/masharti na maumbo yake huwa na viambishi -ki-, -nge-, -ngali-, na -ngeli- Aidha, watahiniwa hao walichagua kipotoshi C “Shurutia kwa kusoma tu sehemu ya kwanza ya swali bila kuangalia kwa makini sehemu ya pili yenye matakwa halisi ya swali. Watahiniwa 50,943 sawa na asilimia 6.67 walichagua kipotoshi E “Mazoea” ambacho pia si jibu sahihi kwa sababu wakati wa mazoea hutambulishwa na kiambishi -hu-.

**Swali la 19:** Mpira umegonga mwamba nusura goli liingie. Neno lipi linaonesha kitendwa?

A Nusura

B Goli

C Mpira

D Mwamba

E Liingie.

**Jedwali 2.17:** Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 69,247 | 128,026 | 146,606 | 346,248 | 69,515 | 3,875 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 9.07 | 16.77 | 19.2 | 45.35 | 9.1 | 0.5 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua kauli za vitenzi. Watahiniwa 346,248 sawa na asilimia 45.35 walichagua jibu D "Mwamba" ambalo ni jibu sahihi kama ilivyo katika Jedwali 2.17. Asilimia 19.2 sawa na watahiniwa 146,606 walichagua kipotoshi C "Mpira" ambacho sio jibu sahihi kwa sababu neno mpira limejitokeza kabla ya kitenzi kikuu "umegonga" chenye umbo la kiambishi tamati "a" kinachoonesha mtenda, hivyo mpira kwa muktadha wa sentensi hiyo siyo mtendwa bali ni mtenda. Watahiniwa 266,788 sawa na asilimia 34.94 walichagua kati ya vipotoshi A "Nusura" B "Goli" na E "Liingie" ambayo si majibu sahihi. Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa "nusura" ni kiunganishi, "goli' ni nomino na "liingie"ni kitenzi. Kwa ujumla watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa sentensi hiyo ilikuwa sentensi ambatano.

**Swali la 20:** Ni neno lipi kati ya haya yafuatayo ni **tofauti** na mengine?

A Sahibu

B Ajuza

C Msiri

D Mwandani

E Mwenzi.

**Jedwali 2.18:** Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 80,533 | 205,573 | 189,370 | 768,68 | 204,644 | 6,529 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 10.55 | 26.92 | 24.8 | 10.07 | 26.8 | 0.86 |

Swali lililenga katika kupima ujuzi wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati. Jedwali 2.18 linaonesha kuwa asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu sahihi ni ndogo kwani watahiniwa 205,573 ambao ni sawa na asilimia 26.92 walichagua B “Ajuza” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya msamiati unaoonesha kinyume cha maneno katika lugha. Uchaguzi wa vipotoshi kati ya A ”Sahibu” C “Msiri” D “Mwandani” na E “Mwenzi” kwa watahiniwa 551,415 ambao ni sawa na asilimia 72 ambayo sio majibu sahihi unaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa misamiati hiyo ina maana sawa kimantiki.

## 2.2 Sehemu B: Lugha ya Kifasihi

**Swali la 21:** Nahau isemayo, “Mtu mwenye ndimi mbili” ina maana ipi kati ya zifuatazo?

A Mropokaji

B Mwongo


C Kilimilimi

D Kigeugeu

E Mfitini.

Swali lililenga kupima tanzu za semi za Kiswahili hasa nahau. Watahiniwa 410,293 sawa na asilimia 53.74 walichagua chaguo D “Kigeugeu” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 348,325 sawa na asilimia 45.62 walichagua kati ya vipotoshi A, B, C na E ambavyo sio majibu sahihi kwa kuwa maneno “mropokaji,” humaanisha msemaji wa maneno mengi yasiyokuwa na maana, “mwongo” lina maana ya mtu asiyesema ukweli “kilimilimi” maana yake ni kuchukua maneno ya upande mmoja na kuyasema sehemu mbalimbali na “mfitini” lina maana ya mchonganishi. Hivyo maneno yote hayo yana mwelekeo wenye maana tofauti na neno “Kigeugeu” ambalo lina maana ya mtu asiye na msimamo thabiti na mwenye kubadili mawazo au kauli mara kwa mara na hivyo kuweza kumfanya awe na mwelekeo hasi au chanya. Kielelezo 2.3 kimeainisha asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Kielelezo 2.3**: Asilimia ya Watahiniwa kwa kila Chaguo




Kielelezo 2.3 kinaonesha kuwa ufaulu ulikuwa ni wa wastani ambapo asilimia 53.74 ya watahiniwa ndio walioweza kuchagua jibu sahihi

**Swali la 22:** Wanafunzi walipotoka safari walilala usingizi wa pono. Msemo usemao, “Usingizi wa pono” una maana gani?

A Usingizi wa mang’amung’amu

B Usingizi wa maruweruwe

C Usingizi mzito mno

D Usingizi wa kustukastuka

E Usingizi wa njozi.

**Jedwali 2.19**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C*** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 101496 | 39575 | 503883 | 65313 | 48987 | 4,263 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.29 | 5.18 | 65.99 | 8.55 | 6.42 | 0.56 |

Swali lililenga kuwapima watahiniwa kuhusu uelewa wa misemo katika lugha ya kifasihi. Jedwali 2.19 linaonesha kuwa swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani asilimia 65.99 ambayo ni sawa na watahiniwa 503,883 walichagua jibu C “Usingizi mzito mno” ambalo ndilo jibu sahihi. Jibu hili ni sahihi kutokana na samaki pono kuwa na usingizi mzito kiasi cha kuvuliwa baharini kwa urahisi. Asilimia 33.44 ambayo ni sawa na watahiniwa 255,371 walichagua vipotoshi kati ya A, B, D na E yaani “Usingizi wa mang’amung’amu”, “Usingizi wa maruweruwe” “Usingizi wa kustukastuka” na “Usingizi wa njozi” ambavyo sio majibu sahihi kwa vile vipotoshi vyote vinaonesha kuwa usingizi huo haukuwa mzito kwa sababu uliingiliwa na vitu vingine kama maruweruwe, kustukastuka na kukosa utimilifu.

**Swali la 23**: Kitendawili kisemacho "Kamba yangu ndefu lakini haiwezi kufunga kuni" kina maana ipi kati ya hizi zifuatazo?

A Mkufu

B Nyoka


C Waya

D Treni

E Njia.

Swali hili lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa katika lugha ya kifasihi na hasa vitendawili. Swali hili ndilo lililojibiwa vizuri na watahiniwa wengi katika mtihani huu ambapo Kielelezo 2.4 kinaonesha kuwa watahiniwa (667,297) sawa na asilimia 87.4 walichagua jibu E "Njia" ambalo lilikuwa ni sahihi. Jibu hili ni sahihi kwa sababu njia ni sehemu inayotumika kupitia kwa mfano, barabara hivyo haiwezi kushikika na kutumika kama kifaa cha kufungia kitu. Tendo la kufunga kuni linawezekana endapo kutakuwepo na kifaa kinachotumika kuviringishwa kwenye kuni na kuweza kuzifunga. Watahiniwa 50,048 sawa na asilimia 6.55 walichagua kati ya vipotoshi A “Mkufu” na B “Nyoka” ambavyo havikuwa majibu sahihi kwa vile mkufu hutumika kufungwa shingoni, nyoka ikiwa na maana ya nyoka mnyama ambaye pia huweza kujiviringisha na hivyo vipotoshi vyote viwili vinaweza kuonesha tendo la kufunga. Aidha, watahiniwa 41,949 sawa na asilimia 5.5 walichagua C “Waya” na D “Treni” ambayo yote sio majibu sahihi kwa sababu waya ambao ni uzi mwembamba wa chuma huweza kufunga vitu na treni ni chombo cha usafirishaji ambacho pia huweza kukutanisha kichwa cha treni na mabehewa mengine hata lile behewa la mwisho. Watahiniwa hawa walishindwa kuhusisha vipotoshi walivyopewa na dhana ya kufunga.

**Kielelezo 2.4:** Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo




Kielelezo 2.4 kinaonesha ufaulu mzuri katika swali la 23 ambapo asilimia 87.4 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.

**Swali la 24:** Methali isemayo "Mgaagaa na upwa hali wali mkavu," inatoa funzo gani?

A Bidii huleta mafanikio

B Mafanikio ni matokeo ya kazi

C Bidii huleta faraja

D Bidii ni kazi ya kuhangaika

E Mafanikio ni ya lazima.

**Jedwali 2.20:** Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 452198 | 137514 | 72880 | 60595 | 35378 | 4,952 |
| Asilimia ya watahiniwa | 59.23 | 18.01 | 9.55 | 7.94 | 4.63 | 0.65 |

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa katika kutambua maana ya methali “Mgaagaa na upwa hali wali mkavu”. Jedwali 2.20 linaonesha kuwa watahiniwa 452,198 sawa na asilimia 59.23 walijibu swali hili vizuri kwa kulichagua chaguo A “Bidii huleta mafanikio” ambalo ndilo jibu sahihi ikiwa na maana kwamba anayetembeatembea kandokando ya bahari hali wali mkavu kwa vile huweza kuokota hata samaki au dagaa na kupata kitoweo. Methali hii inafundisha kuwa anayefanya juhudi katika kazi, masomo au jambo lolote hufanikiwa. Methali hii hutumika kuwashauri na kuwahimiza watu kufanya bidii katika shughuli zao ili wafanikiwe. Aidha, watahiniwa 30,6367 ambao ni sawa na asilimia 40.13 walichagua kati ya vipotoshi B “Mafanikio ni matokeo ya kazi,” C “Bidii huleta faraja,” D “Bidii ni kazi ya kuhangaika” na E “Mafanikio ni ya lazima” jambo linaloonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu maana za methali za Kiswahili.

**Swali la 25**: Usingelitia chumvi kwenye kile kikao wajumbe wasingeligombana. “Kutia chumvi” ni usemi wenye maana gani?

A Kuongeza maneno yenye maudhi

B Kuongeza maneno ya kushtusha

C Kuongeza maneno ya utani

D Kuongeza maneno yenye ukweli

E Kuongeza maneno yasiyo na ukweli.

**Jedwali 2.21:** Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 99890 | 29012 | 43578 | 57930 | 528664 | 4,443 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.08 | 3.8 | 5.71 | 7.59 | 69.24 | 0.59 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua lugha ya kifasihi na hasa nahau. Hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa usahihi na watahiniwa wengi kama inavyoonekana katika Jedwali 2.21, kwani ni watahiniwa 528,664 sawa na asilimia 69.24 ndio waliochagua jibu sahihi E "Kuongeza maneno yasiyo na ukweli" ambayo yana maana sawa na nahau "Kutia chumvi." Watahiniwa 230,410 sawa na asilimia 30.18 walichagua kipotoshi kati ya A, "Kuongeza maneno yenye maudhi" B, "Kuongeza maneno ya kushtusha" C, "Kuongeza maneno ya utani" na D 'Kuongeza maneno yenye ukweli". Uteuzi wa vipotoshi A, B, C na D ambavyo si majibu sahihi unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu maana za misemo ya Kiswahili.

**Swali la 26:** "___________ hufa maskini." Kifungu kipi hukamilisha methali hiyo kwa usahihi?

A Anayeiba cha nduguye

B Anayekula cha nduguye

C Mtegemea cha nduguye


D Mkimbilia cha nduguye

E Asiyethamini cha nduguye.

Swali hili lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu muundo wa methali na hasa kukamilisha methali aliyopewa kwa usahihi.

Watahiniwa wengi (644,045) sawa na asilimia 84.35 walijibu swali hili vizuri kwa kuchagua chaguo C “Mtegemea cha nduguye” ambalo ndilo jibu sahihi. Chaguo hilo linaikamilisha methali hii na kuifanya kuwa na maana kwamba ukitegemea mali aliyonayo ndugu yako, hutopata maendeleo katika maisha kwa kuwa mali ya ndugu yako inamilikiwa na familia yake. Methali hii inawaasa watu kutotegemea mali au kipato cha ndugu kwa kuwa hawatakuwa na mawazo ya kutafuta mali na hatimaye watakuwa maskini milele. Aidha, watahiniwa 116,499 ambao ni sawa na asilimia 15.26 walichagua kati ya vipotoshi A “Anayeiba cha nduguye,” B “Anayekula cha nduguye,” D “Mkimbilia cha nduguye” na E “Asiyethamini cha nduguye” jambo linaloonesha kuwa watahiniwa hao hawana ujuzi wa kutosha kuhusu miundo ya methali za Kiswahili. Kielelezo 2.5 kinaonesha asilimia ya watahiniwa hao kwa kila chaguo.

**Kielelezo 2.5**: Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo




Kielelezo 2.5 kinaonesha kuwa idadi kubwa ya watahiniwa (84.35%) waliweza kubaini jibu sahihi kwa kuchagua chaguo “C”.

**Swali la 27:** Nahau ipi kati ya hizi zifuatazo hutumika kwa watu ambao matendo yao si ya kupendana?

A Kumkubali mtu kwa ulimi tu.

B Hawapikiki katika chungu kimoja.

C Kupaka mafuta kwa mgongo wa chupa.

D Kuvisha kilemba cha ukoka.

E Panya huuma huku akipuliza.

**Jedwali 2.22**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 126,238 | 322,282 | 153,295 | 75,374 | 80,859 | 5,469 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 16.53 | 42.21 | 20.08 | 9.87 | 10.59 | 0.71 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika matumizi ya semi hasa kipengele cha nahau. Jedwali 2.22 linaonesha kuwa idadi ya watahiniwa waliochagua jibu sahihi ilikuwa ya wastani kwani watahiniwa 322,282 sawa na asilimia 42.21 walichagua jibu sahihi ambalo ni B "Hawapikiki katika chungu kimoja" ambayo ni nahau yenye maana kuwa hawapatani/hawaelewani. Watahiniwa 153,295 sawa na asilimia 20.08 walichagua kipotoshi C, "Kupaka mafuta kwa mgongo wa chupa" jibu ambalo si sahihi. Vilevile watahiniwa 75,374 sawa na asilimia 9.87 walichagua kipotoshi D "Kuvisha kilemba cha ukoka" nalo si jibu sahihi. Nahau hizi maana zake ni kumpa mtu sifa asiyostahili wakati unajua wazi kuwa unamhadaa. Watahiniwa 207,097 sawa na asilimia 27.12 walichagua vipotoshi kati ya A na E ambavyo si majibu sahihi. Kipotoshi A "Kumkubali mtu kwa ulimi tu" na maana yake ni kukubali jambo wakati ukijua wazi kuwa hutolitekeleza, maana hii haihusiani kabisa na hali ya kutopendana.

Kipotoshi E “Panya huuma huku akipuliza” maana yake ni hali ya kuwa na unafiki kujifanya unampenda au unamhurumia mtu wakati kwa upande mwingine ndiwe unayepanga njama au unayetoa siri zinazomsababishia matatizo fulani.

**Swali la 28:** Methali ipi kati ya hizi zifuatazo haitoi onyo kuhusu tabia ya mtu?

A Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

B Kiburi si maungwana.

C Mtoto mkaidi mngoje siku ya ngoma.

D Mkaidi hafaidi mpaka siku ya idi.

E Mtoto mwerevu hafunzwi adabu.

**Jedwali 2.23:** Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 81,334 | 79,462 | 209,950 | 92,916 | 294,395 | 5,460 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 10.65 | 10.41 | 27.5 | 12.17 | 38.56 | 0.72 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa katika kutambua methali ambayo haitoi onyo kuhusu tabia ya mtu. Jedwali 2.23 linaonesha kuwa watahiniwa 294,395 sawa na asilimia 38.56 ambao ni chini ya wastani, walichagua chaguo E “Mtoto mwerevu hafunzwi adabu.” Methali hii ina maana kuwa mtoto mwerevu hahitaji kufunzwa adabu kwa kuwa hulishika aambiwalo na kwa kuwa anajua la kufanya hahitaji kuelekezwa kila wakati. Watahiniwa 302,866 sawa na asilimia 39.67 walichagua vipotoshi kati ya C “Mtoto mkaidi mngoje siku ya ngoma” na D “Mkaidi hafaidi mpaka siku ya idi” methali zenye maana kuwa mtu mwenye tabia ya ukaidi na ubishi huzinduka anapopata

matatizo. Watahiniwa 81,334 sawa na asilimia 10.65 walichagua kipotoshi A “Asiyesikia la mkuu huvunjika guu” methali yenye maana kuwa asiyefuata ushauri wa wakubwa au watu wazima hupatwa na madhara. Aidha, watahiniwa 79,462 sawa na asilimia 10.41 walichagua kipotoshi B “Kiburi si maungwana” methali yenye maana kuwa majivuno au maringo sio tabia inayomfaa mtu mwenye heshima na adabu. Vipotoshi A, B, C na D si majibu sahihi kwa sababu vinatoa onyo kuhusu tabia zisizofaa lakini chaguo E ni methali inayoasa kuhusu kuwa na tabia njema.

**Swali la 29:** Methali ipi kati ya hizi zifuatazo inapingana na hii, “umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.”

A Panya wengi hawachimbi shimo

B Kidole kimoja hakivunji chawa

C Palipo na wengi hapaharibiki neno

D Mkono mmoja hauchinji ng’ombe

E Jifya moja haliinjiki chungu.

**Jedwali 2.24**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 322,645 | 199,849 | 106,490 | 58,193 | 71,767 | 4,573 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 42.26 | 26.17 | 13.95 | 7.62 | 9.4 | 0.6 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa kutambua methali ambayo inapingana na methali isemayo, “Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.” Jedwali 2.24 linaonesha kuwa watahiniwa 322,645 sawa na asilimia 42.26 walichagua A “Panya wengi hawachimbi shimo” ambalo ndilo jibu sahihi likiwa na maana kuwa jambo likifanywa na watu

wengi linaweza lisikamilike au lisifanyike vizuri kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa wa watu kutegeana. Watahiniwa 436,299 sawa na asilimia 57.14 walichagua kati ya vipotoshi B “Kidole kimoja hakivunji chawa,” C “Palipo na wengi hapaharibiki neno,” D “Mkono mmoja hauchinji ng’ombe” na E “Jifya moja haliinjiki chungu.” Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa methali hizo zinahimiza kutenda jambo kwa ushirikiano maana ambayo ni sawa na methali “Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.”

**Swali la 30:** “Mchelea mwana kulia hulia yeye mwenyewe.” Methali hii inatoa funzo gani?

A Bora kulea kuliko kulelewa

B Kuhofia kulea si malezi bora

C Mtoto asipofunzwa vema huaibisha

D Kulea mtoto ni kazi kubwa

E Malezi ya mtoto husababisha hofu.

**Jedwali 2.25**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C*** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 189,148 | 80,634 | 403,955 | 52,132 | 32,445 | 5,203 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 24.77 | 10.56 | 52.91 | 6.83 | 4.25 | 0.68 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa wa kutathmini methali aliyopewa. Mtahiniwa alitakiwa kuelezea funzo linalopatikana katika methali isemayo “Mchelea mwana kulia hulia yeye mwenyewe.” Jedwali 2.25 linaonesha kuwa watahiniwa 403,955 sawa na asilimia 52.91 walichagua jibu sahihi ambalo ni C “Mtoto asipofunzwa vema

huaibisha." Watahiniwa 354,359 sawa na asilimia 46.41 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi A "Bora kulea kuliko kulelewa," B "Kuhofia kulea si malezi bora," D "Kulea mtoto ni kazi kubwa" na E "Malezi ya mtoto husababisha hofu" kwa kuwa hawakuwa na uwezo wa kutosha katika kufanya tathmini ya funzo linalopatikana katika methali waliyoulizwa.

## 2.3 Sehemu C: Ufahamu

Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho. Kifuatacho ni kifungu cha habari walichopewa watahiniwa:

> *Matunda kama yalivyo mazao mengine ya kilimo yanatokana na mimea mbalimbali. Kwa mfano fenesi ni tunda litokanalo na mfenesi na chungwa hutokana na mchungwa. Maembe, mapapai, mananasi na mapera ni matunda matamu. Ubuyu, ukwaju na limau ni matunda machachu. Hata hivyo, karibu matunda mengi huwa machachu yakiwa mabichi, yakiiva huwa matamu.*
>
> *Miaka ya hivi karibuni watu wengi wamepanda mimea ya matunda kwenye maeneo ya nyumba zao, hivyo kujipatia matunda kwa njia rahisi. Baadhi ya watu wanaoishi katika mikoa kama vile Tanga na Morogoro wamelima mashamba ya matunda na wameshaona faida ya kilimo hicho na kupanua mashamba yao.*

*Licha ya watu hao kujipatia chakula bora, wameuza matunda na kuwa na pato kubwa.*

*Matunda yana umuhimu mkubwa sana katika miili yetu. Matunda tunayokula yanaikinga miili yetu isipatwe na maradhi. Pia matunda yanaongeza damu mwilini, husaidia kuponyesha vidonda haraka na macho kuona vizuri katika mwanga hafifu. Watu wasiokula matunda hupata udhaifu wa fizi ambao husababisha fizi kutoa damu. Aidha matunda ni kiburudisho wakati wa joto. Watu wengi wamekuwa wakisindika matunda ili kupata juisi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na biashara.*

**Swali la 31:** Kichwa cha habari hii kinachofaa zaidi ni kipi?

A Matunda kwa afya

B Umuhimu wa matunda

C Matunda chanzo cha pato

D Matunda na ulinzi wa mwili

E Matunda hujenga mwili.

**Jedwali 2.26**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 83,383 | 472,062 | 64,658 | 45,669 | 92,628 | 5,117 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 10.92 | 61.83 | 8.47 | 5.98 | 12.13 | 0.67 |

Swali lilipima uwezo wa mtahiniwa wa kuelewa maudhui ya habari aliyoisoma. Jedwali 2.26 linaonesha watahiniwa 472,062 sawa na

asilimia 61.83 walijibu swali vizuri na kwa usahihi kwani waliweza kubaini kichwa cha habari kuwa ni B “Umuhimu wa matunda.” Watahiniwa 286,338 sawa na asilimia 37.5 walichagua kati ya vipotoshi A “Matunda kwa afya,” C “Matunda chanzo cha pato,” D “Matunda na ulinzi wa mwili” na E “Matunda hujenga mwili” ambavyo havikuwa majibu sahihi kwa sababu kila kipotoshi kinaonesha faida moja tu ya matunda wakati habari hii inaelezea faida/umuhimu wa matunda kwa afya na kipato cha mtu.

**Swali la 32:** “Watu wanaokula matunda huepuka magonjwa mengi,” ni methali ipi inaendana na kauli hii?

A Heri kufa macho kuliko kufa moyo.

B Usiache mbachao kwa msala upitao.

C Kinga ni bora kuliko tiba.

D Lisemwalo lipo na kama halipo laja.

E Mwenye kovu usidhani kapoa.

**Jedwali 2.27:** Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C*** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 94,011 | 90,486 | 501,089 | 44,248 | 28,067 | 5,616 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 12.31 | 11.85 | 65.63 | 5.8 | 3.68 | 0.74 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kuhusisha maudhui yanayotokana na kifungu cha habari na methali alizopewa. Jedwali 2.27 linaonesha watahiniwa 501,089 sawa na asilimia 65.63 walichagua jibu sahihi ambalo ni C “Kinga ni bora kuliko tiba” likiwa na maana kuwa ulaji wa matunda humlinda/humkinga mtu dhidi ya magonjwa. Watahiniwa 94,011 sawa na asilimia 12.31 walichagua

kipotoshi A “Heri kufa macho kuliko kufa moyo” jibu ambalo si sahihi. Methali hii maana yake ni afadhali mtu kuwa kipofu kuliko kukata tamaa au kukosa matumaini katika maisha. Watahiniwa 90,486 sawa na asilimia 11.85 walichagua kipotoshi B “Usiache mbachao kwa msala upitao” jibu ambalo si sahihi kwa kuwa methali hii maana yake ni usidharau vitu vya zamani vinavyokufaa kwa kuwa umepata vitu vipya. Aidha, watahiniwa 72,315 sawa na asilimia 9.48 walichagua kati ya vipotoshi D “Lisemwalo lipo na kama halipo laja” na E “Mwenye kovu usidhani kapoa” ambavyo si majibu sahihi. Kipotoshi D ni methali yenye maana kuwa jambo lisemwalo huwa tayari limeshatokea au kama sivyo karibuni litatokea. Hali kadhalika, kipotoshi E ni methali yenye maana kuwa mtu mwenye ubaya fulani halafu akauacha huweza kuurudia au akawa bado anao. Vipotoshi A, B, D na E havina maana inayohusiana na kujikinga au kuwa na tahadhari fulani, bali chaguo C ndilo linaloendana na hali ya kujikinga au kuchukua tahadhari.


**Swali la 33:** Maji ya matunda yaliyokamuliwa huitwaje?

A Mvinyo
B Juisi
C Jusi
D Rozera
E Zabibu.

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati wa Kiswahili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na idadi kubwa ya watahiniwa. Watahiniwa 622,698 sawa na asilimia 81.56 walichagua B “Juisi” ambalo ndilo

jibu sahihi. Watahiniwa 38,257 sawa na asilimia 5.01 walichagua kipotoshi A “Mvinyo” ambalo si jibu sahihi kwa kuwa mvinyo ni kileo kinachotengenezwa kwa maji ya matunda. Watahiniwa 40,836 sawa na asilimia 5.35 walichagua kipotoshi C “Jusi” ambalo si jibu sahihi, jusi ni nomino iliyopatikana kutokana na nomino “mjusi” kuwekwa katika dhana ya ukubwa/ukubwaishi hivyo “jusi” ni mjusi mkubwa. Watahiniwa 58,285 sawa na asilimia 7.64 walichagua vipotoshi D “Rozela” na E “Zabibu” ambayo ni matunda na si maji ya matunda yaliyokamuliwa. Uchaguzi huo unaonesha kuwa, watahiniwa walipotoshwa na dhana ya matunda yanayoweza kukamuliwa na kupata juisi kwa kuwa rozela na zabibu huweza kukamuliwa na kupata juisi. Kwa ujumla watahiniwa wengi walikuwa na ufaulu mzuri katika swali hili kama inavyoonekana katika Kielelezo 2.6.

**Kielelezo 2.6:** Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo




Kielelezo 2.6 kinaonesha ufaulu wa swali hili ulikuwa mzuri ambapo asilimia 81.56 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi.

**Swali la 34:** "Matunda yaliyoiva" ina maana sawa na ipi kati ya zifuatazo?

A Yenye ukakasi

B Machachu


C Matamu

D Mabichi

E Mabivu.

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati. Hili ni swali lililojibiwa vibaya kuliko maswali mengine yote katika mtihani huu, kwani ni watahiniwa 152,610 sawa na asilimia 19.99 tu ndio waliochagua jibu sahihi E “Mabivu” lenye maana sawa na yaliyoiva. Idadi kubwa ya watahiniwa (512,407) sawa na asilimia 67.11 walichagua kipotoshi C “Matamu” lenye maana zifuatazo: yenye ladha ya sukari, yenye ladha ya kuridhisha kinywani, yenye kufurahisha. Jibu hili si sahihi kwa sababu kipotoshi “Matamu” kinaelezea dhana ya ladha na sio kuiva/kupevuka kwa matunda. Aidha, katika hali halisi si matunda yote yanapoiva yanakuwa na ladha ya utamu. Watahiniwa 95,270 sawa na asilimia 12.47 walichagua kati ya vipotoshi A “Yenye ukakasi,” B “Machachu” na D “Mabichi” ambavyo si majibu sahihi. Uteuzi wa vipotoshi A, B, C na D ambavyo si majibu sahihi unaonesha kuwa watahiniwa hao ambao ni sawa na asilimia 79.58 hawana ujuzi wa kutosha kuhusu maana za misamiati ya Kiswahili. Kielelezo 2.7 kinaonesha asilimia ya watahiniwa kwa kila jibu.

**Kielelezo 2.7**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo




Kielelezo 2.7 kinaonesha ufaulu hafifu ambapo asilimia 19.99 ya watahiniwa ndio walioweza kuchagua jibu sahihi.

**Swali la 35:** "Kilimo cha matunda kimekuwa cha faida kubwa kwao." Methali ipi ambayo inaendana na maelezo hayo?

A Jembe halimtupi mtu.

B Mla ni mla leo mla jana kala nini.

C Jisaidie Mungu akusaidie.

D Mchumia juani hulia kivulini.

E Kula nanasi kwahitaji nafasi.

**Jedwali 2.28:** Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 284,997 | 44,585 | 65,161 | 334,713 | 30,898 | 3,163 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 37.33 | 5.84 | 8.53 | 43.84 | 4.05 | 0.41 |

Swali lilikuwa linampima mtahiniwa kuhusu uelewa wa maudhui au ujumbe wa habari kwa ujumla. Jedwali 2.28 kinaonesha kuwa watahiniwa 284,997 sawa na asilimia 37.33 walijibu swali kwa usahihi kwa kubaini methali inayoendana na kauli "Kilimo cha matunda kimekuwa cha faida kubwa kwao" ambayo ni A "Jembe halimtupi mtu." Methali hii ina maana kuwa mtu anayefanya kazi kwa bidii mathalani kulima kwa bidii hakosi mafanikio. Mwandishi wa habari hii anakisifu kilimo cha matunda na kuonesha jinsi kilivyoinua maisha ya watu. Watahiniwa 334,713 sawa na asilimia 43.84 walichagua kipotoshi D "Mchumia juani hulia kivulini" methali yenye maana kuwa mtu anayefanya kazi ngumu huishia kufurahia mafanikio yake. Methali hii si jibu sahihi kwa sababu kulima si kazi ngumu kwa sababu kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia mashine hutumika katika shughuli ya kilimo. Aidha, mkulima si lazima atumie nguvu zake katika kulima anaweza kuajiri vibarua. Watahiniwa 140,644 sawa na asilimia 18.42 walichagua kati ya kipotoshi B "Mla ni mla leo mla jana kala nini," C "Jisaidie Mungu akusaidie" na E "Kula nanasi kwahitaji nafasi" ambayo sio majibu sahihi. Maana za methali hizi haziendani na kauli kuwa "Kilimo cha matunda kimekuwa cha faida kubwa kwao" kwani methali isemayo "Mla ni mla leo mla jana kala nini," maana yake ni mtu mwenye uwezo/mali leo ndiye anayeheshimika wala si yule aliyekuwa na uwezo/mali jana au zamani. Methali isemayo "Jisaidie Mungu akusaidie" maana yake ni

fanya jitihada katika maisha badala ya kulalamika tu au kungoja Mungu akusaidie. Aidha, methali isemayo "Kula nanasi kwahitaji nafasi" maana yake ni kupata mafanikio katika maisha kunahitaji juhudi na uvumilivu kama ilivyo unapotaka kula nanasi ambalo lina usumbufu katika kulimenya.

**Swali la 36:** Ni kwanini wakulima wa matunda hupanua mashamba yao?

A Kupata chakula

B Kupata kiburudisho

C Kuongeza pato

D Kupata sifa

E Kupata mikopo.

**Jedwali 2.29**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C*** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 105,886 | 46,199 | 565,688 | 21,466 | 21,456 | 2,822 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.87 | 6.05 | 74.09 | 2.81 | 2.81 | 0.27 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa katika kusoma na kuelewa mawazo makuu yatokanayo na habari aliyoisoma. Watahiniwa 565,688 sawa na asilimia 74.09 waliielewa habari na kuweza kuchagua jibu sahihi C "Kuongeza pato" kama inavyoonekana katika Jedwali 2.29. Watahiniwa hao pia waliweza kuhawilisha maarifa yaliyomo katika kifungu cha habari hususan katika aya ya pili mstari wa saba ambao unaelezea faida za kilimo cha matunda. Uteuzi wa vipotoshi A "Kupata chakula", B "Kupata kiburudisho", D "Kupata sifa" na E "Kupata mikopo" uliofanywa na

watahiniwa 195,007 sawa na asilimia 25.54 unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu namna ya kupata mawazo makuu ya habari waliyoisoma.

**Swali la 37:** Matunda ya ubuyu na ukwaju yakiwa yameiva huwa na ladha gani?

A Chumvi

B Uchungu

C Ukakasi

D Ukali

E Uchachu.

**Jedwali 2.30**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D** | **E*** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 38,821 | 47,976 | 88,220 | 35,949 | 547,961 | 4,590 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 5.08 | 6.28 | 11.55 | 4.71 | 71.77 | 0.28 |

Swali lilipima uwezo wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati. Jedwali 2.30 linaonesha kuwa watahiniwa wengi (547,961) ambao ni asilimia 71.77 walijibu swali hili vizuri kwa kuchagua jibu E "uchachu" ambalo ndilo jibu sahihi. Uteuzi wa vipotoshi A "Chumvi," B "Uchungu," C "Ukakasi" na D "Ukali" uliofanywa na watahiniwa 210,966 sawa na asilimia 27.62 unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kuhawilisha maudhui yaliyomo katika kifungu cha habari walichopewa. Katika kifungu cha habari ladha ya "ubuyu" na "ukwaju" imetajwa wazi katika aya ya kwanza mstari wa tano na wa sita.

**Swali la 38:** Kazi kubwa ya matunda mwilini ni ipi?

A Kuponyesha macho

B Kuburudisha

C Kujenga mwili

D Kuponyesha vidonda

E Kulinda mwili.

**Jedwali 2.31**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D** | **E*** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 41,398 | 34,383 | 157,639 | 133,677 | 392,393 | 4,027 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 5.42 | 4.5 | 20.65 | 17.51 | 51.39 | 0.53 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kuelewa maudhui yaliyomo katika kifungu cha habari alichopewa. Jedwali 2.31 linaonesha kuwa watahiniwa 392,393 sawa na asilimia 51.39 walichagua jibu E "Kulinda mwili" ambalo ni sahihi. Matunda hulinda mwili dhidi ya maradhi mbalimbali kama ilivyoelezwa katika aya ya tatu mstari wa kwanza na wa pili. Watahiniwa 209,458 sawa na asilimia 27.43 waliteua vipotoshi A "Kuponyesha macho," B "Kuburudisha" na D "Kuponyesha vidonda" ambavyo si majibu sahihi. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa kazi hizo zote kwa ujumla wake ni kulinda mwili dhidi ya magonjwa. Uteuzi wa kipotoshi C "Kujenga mwili" uliofanywa na watahiniwa 157,639 sawa na asilimia 20.65, unaonesha kuwa watahiniwa hao hawana maarifa ya kutosha kuhusu kazi za aina mbalimbali za vyakula. Matunda ni vitamini hivyo kazi yake kubwa ni kuulinda mwili, kazi ya kujenga mwili hufanywa na vyakula ambavyo ni vya aina ya protini.

**Swali la 39:** "Kusindika matunda" ina maana sawa na kifungu kipi kati ya vifuatavyo?

A Kusaga na kukamua matunda
B Kukamua matunda na kuyahifadhi
C Kukamua na kuchuja matunda
D Kuyasaga matunda yaliyoiva
E Kuyaivisha matunda na kuyasaga.

**Jedwali 2.32**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 157,188 | 239,310 | 165,562 | 88,782 | 10,6711 | 5,964 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 20.59 | 31.34 | 21.68 | 11.63 | 13.98 | 0.78 |

Swali lilipima uwezo wa mtahiniwa katika kutumia msamiati wa lugha ya Kiswahili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya na watahiniwa wengi kama inavyoonekana katika Jedwali 2.32. Watahiniwa 157,188 tu sawa na asilimia 20.59 walichagua A ambalo ndilo jibu sahihi "Kusaga na kukamua matunda." Kusindika ni kusaga na kukamua mbegu au tunda la mti au mmea fulani ili kutoa umajimaji uliomo katika kitu hicho. Watahiniwa wengi (600,365) sawa na asilimia 78.63 walijibu swali hili vibaya kwa kuchagua vipotoshi kati ya B "Kukamua matunda na kuyahifadhi," C "Kukamua na kuchuja matunda," D "Kuyasaga matunda yaliyoiva" na E "Kuyaivisha matunda na kuyasaga." Majibu hayo hayakuwa sahihi kwa sababu dhana ya kusindika ni lazima kuwe na tendo la kusaga na kukamua kwa wakati mmoja.

**Swali la 40:** Umepata funzo gani kutokana na kifungu hiki cha habari?

A Matunda hukuza akili.

B Matunda huongeza unene.

C Matunda hukuza akili na mwili.

D Matunda hulinda mwili na huongeza damu.

E Matunda hujenga mwili na huongeza joto.

**Jedwali 2.33**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D*** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 25,290 | 33,299 | 38,361 | 589,110 | 72,789 | 4,668 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 3.31 | 4.36 | 5.02 | 77.16 | 9.53 | 0.61 |

Swali lilipima uwezo wa mtahiniwa katika kutathmini funzo alilolipata katika kifungu cha habari alichokisoma. Watahiniwa wengi sawa na asilimia 77.16 kama inavyoonekana katika Jedwali 2.33 walijibu swali hili vizuri kwa kuchagua D “Matunda hulinda mwili na huongeza damu” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa hawa wameweza kuhusisha kazi kuu ya matunda katika mwili wa mwanadamu, kuwa ni kulinda mwili dhidi ya magonjwa mbalimbali na pia huongeza damu. Watahiniwa 169,739 sawa na asilimia 22.22 walichagua kati ya vipotoshi A “Matunda hukuza akili”, B “Matunda huongeza unene,” C “Matunda hukuza akili na mwili” na E “Matunda hujenga mwili na huongeza joto.” Uteuzi wa vipotoshi hivyo unadhihirisha udhaifu wa watahiniwa hao katika ujengaji wa mawazo ya jumla baada ya kusoma kifungu cha habari. Kazi zilizotajwa katika vipotoshi hivyo hazihusiani na kazi za matunda katika mwili wa binadamu.

## 2.4 Sehemu D: Ushairi

Katika sehemu hii watahiniwa walitakiwa kusoma shairi lifuatalo na kujibu maswali yanayotokana na shairi hilo

*Mtu kujitegemea, huwa jambo la lazima,*
*Usipende subiria, kusaidiwa daima,*
*Huwezi kuendelea, ndugu usipojituma,*
*Kamwe hupati heshima, usipojitegemea.*

*Kama Mungu kakuumba, mzima huna kilema,*
*Fedheha kuombaomba, takuwa mtu wa nyuma,*
*Hutakuja kujigamba, ukikudharau umma,*
*Kamwe hupati heshima, usipojitegemea.*

*Kazi mtu usidhani, sharti ni ya kusoma,*
*Ya kuleta ofisini, na kuhesabu ndarama,*
*Waweza kwenda shambani, ushike jembe kulima,*
*Kamwe hupati heshima, usipojitegemea.*

*Utaambiwa doezi, mtu uso taadhima*
*Pengine uitwe mwizi, umezoea dhuluma*
*Wajapo wapelelezi, ndiwe watakuandama*
*Kamwe hupati heshima, usipojitegemea*

**Swali la 41**: Katika shairi ulilosoma neno “ndarama” lina maana ipi?

A Mali

B Pesa

C Gharama

D Amana

E Thamani.

**Jedwali 2.34**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 91063 | 451629 | 133678 | 33695 | 48775 | 4,677 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 11.93 | 59.15 | 17.51 | 4.41 | 6.39 | 0.62 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati kama ulivyotumika katika shairi. Jedwali 2.34 linaonesha kuwa watahiniwa 451,629 sawa na asilimia 59.15 walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu B “Pesa” ambalo ndilo lilikuwa na maana sawa na neno “ndarama.” Aidha, watahiniwa 307,211 sawa na asilimia 40.24 walichagua vipotoshi kati ya A, C, D na E, ambavyo sio majibu sahihi. Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha maana ya neno “ndarama” na maneno kama vile “Mali” ambalo maana yake ni kitu au vitu vyenye thamani kubwa alivyo navyo mtu, “Gharama” ni kitu kinachotolewa hasa pesa ili kulipia vitu au huduma. Pia “Amana” lenye maana ya kitu chenye thamani kubwa. Aidha, neno “Thamani” lenye maana ya bei ya kitu. Kwa ujumla maneno yaliyomo katika vipotoshi A, C, D na E yana maana ambayo ni tofauti na neno ndarama.

**Swali la 42:** Kisawe cha neno “taadhima” ni kipi?

A Heshima
B Taashira
C Dhamiri
D Dhima
E Dhamana.

**Jedwali 2.35**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 489128 | 68920 | 82966 | 38559 | 78880 | 5,064 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 64.06 | 9.03 | 10.87 | 5.05 | 10.33 | 0.66 |

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu visawe vya maneno ya Kiswahili. Watahiniwa wengi (489,128) sawa na asilimia

64.06 kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali 2.35 walichagua jibu A "Heshima" ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 269,325 sawa na asilimia 35.28 walichagua kati ya vipotoshi B, C, D na E ambavyo sio majibu sahihi, hali inayoonesha kuwa watahiniwa walishindwa kuelewa maana ya neno "Taashira" ambalo lina maana ya ishara au dalili. Aidha, neno "Dhamira" likiwa na maana ya mawazo yanayomfanya mtu kufanya jambo zuri au baya na neno "Dhima" ambalo lina maana ya wajibu mkubwa, uwezo wa kufanya jambo au madaraka. Hali kadhalika, neno "Dhamana" lina maana ya kitu au ahadi inayotolewa kumdhamini mtu anayetaka kukopa mali au anayekabiliwa na mashitaka mahakamani. Hivyo watahiniwa hao hawakuwa na uelewa unaotakiwa wa visawe sahihi vya neno "taadhima". Kwa ujumla, watahiniwa hao walishindwa kuelewa maana ya neno "taadhima" ili kuweza kupata kisawe sahihi.

**Swali la 43**: Ujumbe unaopatikana katika shairi hili unaweza kuwasilishwa kwa methali ipi kati ya zifuatazo?

A Mkulima ni mmoja walaji ni wengi

B Mchagua jembe si mkulima

C Mkulima hasahau jembe kiserema

D Mkulima halaumu jembe lake

E Kilimia kikizama kwa jua huibuka kwa mvua.

**Jedwali 2.36**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 178631 | 341355 | 72682 | 73833 | 90452 | 6564 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 23.4 | 44.71 | 9.52 | 9.67 | 11.85 | 0.86 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa katika kubaini maudhui ya shairi alilolisoma. Jedwali 2.36 linaonesha kuwa watahiniwa 341,355 sawa na asilimia 44.71 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walikuwa na uelewa wa maudhui yanayopatikana katika shairi hilo, hivyo waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo lilikuwa B "Mchagua jembe si mkulima". Katika shairi hili jamii inahimizwa kufanya kazi na isipende kuchagua kazi. Watahiniwa 414,598 sawa na asilimia 54.39 waliochagua vipotoshi A, C, D na E hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu namna ya kupata ujumbe katika kazi za fasihi, hasa namna ya kupata maudhui ya kazi za fasihi hususan maudhui ya shairi.

**Swali la 44**: Katika shairi ulilosoma kituo bahari ni kipi?

A Mtu kujitegemea, huwa jambo la lazima.

B Kama Mungu kakuumba, mzima huna kilema.

C Utaambiwa doezi, mtu uso taadhima.

D Waweza kwenda shambani, ushike jembe kulima.

E Kamwe hupati heshima, usipojitegemea.

**Jedwali 2.37**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 101363 | 69601 | 52462 | 46646 | 487333 | 6,112 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.28 | 9.12 | 6.87 | 6.11 | 63.83 | 0.8 |

Swali lilikuwa linapima maarifa ya mtahiniwa kuhusu kanuni za utunzi wa shairi. Swali lilijibiwa kwa usahihi na watahiniwa wengi (487,333) ambao ni sawa na asilimia 63.8 kama inavyoonekana katika Jedwali 2.37 walichagua jibu sahihi ambalo ni E "Kamwe hupati heshima, usipojitegemea." Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu utunzi wa mashairi hasa dhana ya kituo. Watahiniwa 223,426 sawa na asilimia 29.27 walichagua kati ya vipotoshi A, B na C kwa kuwa walihusisha mstari wa kwanza katika ubeti wa 1, 2 na wa 3 kama kituo cha shairi na walishindwa kutambua kuwa kituo ni mstari wa mwisho. Watahiniwa 46,646 sawa na asilimia 6.11 walichagua D "Waweza kwenda shambani, ushike jembe kulima" kwa kuhusisha mstari wa tatu katika ubeti wa tatu kama kituo cha shairi. Kwa ujumla watahiniwa hao waliochagua kati ya vipotoshi A, B, C na D ambavyo sio majibu sahihi hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu kanuni za utunzi wa shairi na hasa muundo wa kituo katika shairi.

**Swali la 45**: Katika shairi ulilosoma nusu mstari una mizani ngapi?

A Nane
B Mbili
C Tatu
D Nne
E Kumi na tano.

**Jedwali 2.38**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 478376 | 70548 | 42263 | 102168 | 64847 | 5315 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 62.65 | 9.24 | 5.54 | 13.38 | 8.49 | 0.7 |

Swali lilikuwa linapima maarifa ya mtahiniwa kuhusu kanuni za utunzi wa shairi. Swali lilijibiwa kwa usahihi na watahiniwa 478,376 sawa na asilimia 62.65 kama inavyoonekana katika jedwali 2.38. Watahiniwa hao walichagua jibu sahihi ambalo ni A “Nane.” Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu utunzi wa mashairi hasa idadi kamili ya mizani katika kila nusu mstari. Watahiniwa 70,548 sawa na asilimia 9.24 walichagua kipotoshi B “Mbili” kwa kuwa walihusisha idadi ya mistari miwili katika kila ubeti kwa vile kila mstari umegawanywa mara mbili kila baada ya mizani nane. Watahiniwa 42,263 sawa na asilimia 5.54 walichagua kipotoshi C “Tatu” kwa kuhusisha mistari mitatu iliyopo katika kila ubeti kabla ya kituo. Aidha, watahiniwa 102,168 ambao ni sawa na asilimia 13.38 walichagua kipotoshi D “Nne” kwa kuhusisha idadi ya mistari katika kila ubeti. Pia watahiniwa 64,847 walichagua kipotoshi E “Kumi na tano” kwa kushindwa kutambua kanuni za utunzi wa ushairi kwa vile idadi hiyo haijitokezi popote katika beti za shairi hilo. Kwa ujumla uteuzi wa vipotoshi ambavyo si majibu sahihi unaonesha wazi kuwa watahiniwa hao hawana ujuzi wa kutosha kuhusu kanuni za utunzi wa mashairi.

**Swali la 46**: Neno “fedheha” kama lilivyotumika katika shairi hili lina maana gani?

A Maudhi
B Lawama
C Adibu
D Adhibu
E Aibu.

**Jedwali 2.39**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 102833 | 154859 | 51026 | 38888 | 409192 | 6719 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.47 | 20.28 | 6.68 | 5.09 | 53.59 | 0.88 |

Swali lilikuwa linapima matumizi ya msamiati kama ulivyotumika katika shairi. Jedwali 2.39 linaonesha kuwa watahiniwa 409,192 sawa na asilimia 53.59 walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu E "Aibu" ambalo ndilo lilikuwa na maana sawa na neno "fedheha". Aidha, watahiniwa 347,606 sawa na asilimia 45.52 walichagua kati ya vipotoshi A "Maudhi" ambalo maana yake ni karaha au maneno yanayomfanya mtu akasirike, B "Lawama" likiwa na maana ya maneno yatolewayo kwa kutokuridhishwa na jambo, C "Adibu" ambalo maana yake ni kufundisha mwenendo mwema na D "Adhibu" ambalo maana yake ni kutesa mtu kutokana na makosa aliyoyafanya. Vipotoshi A, B, C na D ambavyo vyote havikuwa majibu sahihi vinaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kutofautisha maana ya neno "fedheha" na maana za vipotoshi hivyo.

## 2.5 Sehemu E: Utungaji

Katika sehemu hii, watahiniwa walipewa habari yenye sentensi nne (4) zilizoandikwa bila mtiririko sahihi na walitakiwa wazipange sentensi hizo ili ziwe na mtiririko wenye mantiki kwa kuzipa herufi A, B, C na D.

**Swali la 47:** Ukataji miti kwa wingi kwa ajili ya ujenzi na shughuli zingine huweza kuisababishia nchi yetu ya Tanzania kuwa jangwa.

**Swali la 48:** Kutokana na miti watu hujenga nyumba nzuri za kila namna, zinazopendeza na za kudumu.

**Swali la 49:** Hivyo ni muhimu kwa kila mtu kupanda mti kila anapokata mti kwani nchi isiyo na miti ni sawa na mtu ambaye amevuliwa nguo.

**Swali la 50:** Miti ina faida nyingi sana kwa binadamu.

**Jedwali 2.40**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo

| Swali | Jibu sahihi | Idadi ya watahiniwa | Asimilia ya watahiniwa | Mengine (%) | Jibu E (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| **47** | **C** | 338,432 | 44.33 | 0.53 | 3.24 |
| **48** | **B** | 384,310 | 50.33 | 0.48 | 2.37 |
| **49** | **D** | 326,899 | 42.81 | 0.47 | 3.2 |
| **50** | **A** | 529,665 | 69.37 | 0.36 | 2.66 |

Swali hili lililenga kupima uwezo wa watahiniwa katika upangaji wa mawazo katika mtiririko wenye mantiki. Jedwali 2.40 linaonesha kuwa watahiniwa 338,432 ambao ni asilimia 44.33 waliweza kuandika sentensi ya kwanza kwa usahihi kama ilivyotakiwa. Hata hivyo asilimia iliongezeka katika upangaji wa sentensi ya pili kwani watahiniwa 384,310 sawa na asilimia 50.33. walipanga sentensi hiyo kwa usahihi. Upangaji wa sentensi ya tatu haukufanyika vizuri sana kwani ni watahiniwa 326,899 tu sawa na asilimia 42.81 ndio walioandika sentensi hiyo kwa usahihi. Katika kukamilisha sentensi ya mwisho idadi na asilimia ya watahiniwa iliongezeka na kufikia watahiniwa 529,665 sawa na asilimia 69.37. Asilimia 2.66 hadi 3.24

walijibu maswali haya kama yale ya kuchagua kwa kujaza kipengele E ambacho hakikuwepo katika sehemu hii ya mtihani. Watahiniwa hawa hawakuelewa maelekezo ya swali na pia inaelekea kuwa walikuwa wanachagua majibu bila kusoma kilichoandikwa kwani wangekuwa wanasoma wangebaini kuwa herufi E haikuwa miongoni mwa herufi walizopaswa kuziandika katika swali hilo.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI

Mtihani wa Kiswahili ulitahini mada tano ambazo ni Sarufi, Lugha ya Kifasihi, Ufahamu, Ushairi na Utungaji. Uchambuzi unaonesha kuwa katika kila mada kuna maswali yaliyojibiwa vizuri na idadi kubwa ya watahiniwa lakini pia yapo yaliyojibiwa vibaya na idadi kubwa ya watahiniwa. Kwa upande wa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa ni swali la 23 kutoka katika mada ya Sarufi na swali la 26 kutoka katika mada ya Lugha ya Kifasihi, ambapo kwa swali la 23 watahiniwa 667,297 sawa na asilimia 87.4 na kwa swali la 26 watahiniwa 644,045 sawa na asilimia 84.35 waliweza kuchagua majibu sahihi. Swali moja kutoka katika mada ya Ufahamu pia lilijibiwa vizuri yaani swali la 33 ambalo lilijibiwa vizuri na watahiniwa 622,698 sawa na asilimia 81.56. Hali kadhalika, swali la 40 lililotoka katika mada ya Ufahamu lilijibiwa vizuri na watahiniwa 589,110 sawa asilimia 77.16. Aidha, kwa upande wa maswali yaliyojibiwa vibaya ni kama vile, swali la 34 kutoka mada ya Ufahamu ambapo ni asilimia 19.99 tu ya watahiniwa ndio walioweza kuchagua jibu sahihi. Swali hili lilijibiwa vibaya kuliko maswali mengine yote katika mtihani huu. Swali la 12 kutoka mada ya Sarufi nalo lilikuwa na asilimia ndogo ya watahiniwa waliojibu kwa usahihi, kwani ni watahiniwa 155,295 sawa na asilimia 20.34 ndio

waliochagua jibu sahihi. Vile vile ufaulu mdogo ulijitokeza katika swali la 20 na 39 yaliyotoka katika mada ya Sarufi na Ufahamu mtawalia, ambapo kwa swali la 20 watahiniwa 205,573 sawa na asilimia 26.92 ndio waliochagua jibu sahihi na swali la 39 watahiniwa 157,188 sawa na asilimia 20.59 tu ndio waliojibu swali hilo kwa usahihi. Uchambuzi wa mada umebaini kuwa wastani wa ufaulu kwa mada umeongezeka katika mada zote kwa asilimia kati ya 1.01 hadi 13.81. Japokuwa kumekuwa na ongezeko la wastani wa ufaulu katika kila mada, bado juhudi zaidi zinahitajika katika ujifunzaji na ufundishaji wa mada zote ili kiwango cha ufaulu kiongezeke kutoka wastani na kuwa kizuri. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa kwa kila mada katika somo la Kiswahili umewasilishwa katika **Grafu**.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa namna watahiniwa walivyojibu maswali unaonesha changamoto mbalimbali ambazo watahiniwa walikumbana nazo walipokuwa wakifanya mtihani. Changamoto hizo ni pamoja na kushindwa kutambua matakwa ya swali, kuwa na uelewa mdogo wa mada mbalimbali katika somo; kutofahamu kanuni za lugha na matumizi ya misamiati na kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo katika mtihani.

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu kwa kila mada kimekuwa ni cha wastani kama kilivyokuwa kwa mwaka 2014. Hata hivyo, kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2015 wastani wake umeongezeka na kuwa asilimia 37.12 ambao una ongezeko la asilimia 17.4 ukilinganishwa na wa mwaka 2014 ambao ulikuwa 20.32. Uchambuzi wa mada umebaini kuwa wastani wa ufaulu kwa mada umeongezeka katika

mada zote. Ongezeko hilo ni kati ya asilimia 1.01 hadi 13.81. Pamoja na kuwepo na ongezeko la wastani wa ufaulu katika kila mada, bado juhudi zaidi zinahitajika katika ujifunzaji na ufundishaji wa mada zote ili kiwango cha ufaulu kiongezeke kutoka wastani na kuwa kizuri.

Kutokana na uchambuzi huu, inaonesha wazi kuwa suala la ujifunzaji na ufundishaji wa somo la Kiswahili kwa shule za msingi linatakiwa lifanyike kwa ukamilifu ili kuwawezesha wanafunzi kutumia Kiswahili fasaha. Kwa kupitia wadau mbalimbali wa lugha ya Kiswahili, somo hili linatakiwa kupewa kipaumbele kwa kuwawezesha wanafunzi kupata maarifa ya kutosha kuhusu somo la Kiswahili ili waweze kukabiliana na changamoto mbalimbali za kitaaluma na za kimaisha kuhusiana na lugha ya Kiswahili.

Itambulike wazi kuwa Kiswahili ni lugha ya Taifa, ni sehemu ya utamaduni wa Mtanzania na ni lugha inayoziunganisha nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na pia hutumika kimataifa. Hivyo, ni vyema juhudi endelevu za kuinua lugha hii zifanyike kuanzia shule za msingi hadi elimu ya juu. Kwa kufanya hivi, lugha hii ya Kiswahili itakuwa imetendewa haki na kupewa hadhi inayostahili katika taifa hili.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuwawezesha watahiniwa kupata maarifa na ujuzi wa kutosha na pia katika kuboresha matokeo yao katika mtihani wa Kiswahili mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa:

(a) Walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule za msingi wanatakiwa kufundisha mada zote kwa ukamilifu kama ilivyoelekezwa katika muhtasari.

(b) Ili kupata ujifunzaji na ufundishaji wenye mafanikio, walimu wanatakiwa kutoa mazoezi ya kutosha kwa wanafunzi kuhusiana na mada mbalimbali wanazofundisha, ikiwa ni pamoja na kuwapa wanafunzi mrejeo wa matokeo ya mazoezi hayo kila mara.

(c) Wanafunzi wajengwe kifikra kuhusu umuhimu wa kusoma vitabu mbalimbali vya hadithi ambavyo vitawajengea ujuzi katika uchambuzi ulio makini wa vifungu mbalimbali katika mada ya ufahamu.

(d) Wanafunzi wahamasishwe katika kutumia Kiswahili sanifu katika mazungumzo na maandishi yao ya kila siku ili kuboresha misamiati na sarufi ya lugha ya Kiswahili kwa ujumla.

**KIAMBATISHO CHA PEKEE**

## ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA KATIKA PSLE 2015 NA PSLE 2014 SOMO LA KISWAHILI

